“Yesu Kristo Niyeye yule Jana na leo na hata milele”
(Waebrania 13: 8)

# Barua Ya Muzunguko Decemba 2020

Salamu za kujaa moyo kwa wandugu na wadada wote ulimwenguni pote katika jina tukufu la BWANA na Mwokozi wetu Yesu Kristo na andiko kutoka 1 Yohana 2, shahiri la 27:

*“Nanyi mafuta yale muliopata kwake yana kaa ndani yenu, wala hamnahaja ya mtu kuwa fundisha; lakini kama mafuta yae yanavyo wafundisha kweli wala si uongo, na kama yalivyowafun-disha, kaeni ndani yake.”*

Maneno haya yaweze kupenya kilindini katika kila moyo nakuwa kweli. Chini ya upako wa hapo hapo na uvuviyo wa Roho Mtakatifu, manabii wali weza kueleza mpango waokovu mbele katika neno la Mungu. Hiyo upako moja moja ili kuwa ku mwokozi wetu. Alikuwa Kristo-Mupakaliwa. Katika Luka 4:18-19 Mwokozi wetu alisoma andiko katika Isaya 61, shahiri ya kwanza na kipande cha shahiri ya 2: *“Roho wa Bwana yu juuu yangu, kwa maana amenitiya mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwa tangaziya wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwa aacha huru walio teseka, Na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubali.*“ Nasi kama waamini wa kweli tume pokeya yule Roho moja, hiyo upako moja, mafundisho mamoja, hiyo ufunuo moja wa Yesu Kristo.

Paulo alikuwa na mwito wa hapo hapo, alikuwa chini ya upako na uvuviyo wa Roho wa Mungu, na alikuwa na uhakika kwa utangazaji ambayo ange pashwa sema, “Mtu yeyote anaye hubiri injili nyengine yiko nichini ya laana.” (Gal 1:8) William Branham, mtu wa Mungu kwa wakati wetu, naye alikuwa na mwito wa kiungu wa hapo hapo, alikuwa chini yaupaka na uvuviyo wa Roho Mtakatifu, na alihubiri injili ya milele. Hiyo ni kweli kulingana na mwito wangu. Kama vile BWANA Mungu anatangazaka mwito, yeye kila mara ana kuwaka natumaini ndani ya manabii, mitume, na watumishi wa Mungu ambao amewaweka katika huduma. Neno

ambalo BWANA alisema ndani ya Yohana 20:21 lingalii na shikiliya mpka leo*: "Basi Yesu akawaambiya tena, Amani iwe kwenu; Kama baba alivyo nituma mimi, miminanyi nawa peleka ninyi."* Kutuma kwa kiungu ina kuwaka ina k tena na yale ambayo BWANA wetu alisema katika Yohana 13:20: *"Amin, Amin, nawaambieni, yeye ampokeyaye mtu yeyote nimpelekaye, anipokea mimi, naye anipokeaye mimi, ampokea yeye aliyenipeleka."*

Katika maandiko iliyo nukuliwa kati kujitambulisha kwetu, mtume Yohana aliandika kwamba upako una endeleya kuduma ndani ya mtoto wa Mungu wa kweli. Alio onyesha vema kwamba hakuna uongo unayo tokandani ya kweli (shahiri ya 21). Nahata tangu shahiri la 20 tunasoma: *"Nanyi mmepakwa mafuta nayeye aliye mutakatifu nanyi mnajua yote."* Maneno yake katika shahiri la 28 yalikuwa na onyeshwa kwetu kwa hiyi wakati: *"Na sasa, watoto wadogo, kaeni ndani yake, ili kusudi, atakapofunuliwa, muwe na ujasiri wala musiaibike mbele zake katika kuja kwake."* (1 Yohane 2:28).

Sisi sote twangojea ufunuo wa Yesu Kristo na tuna taka kuwa tayari wakati wa kurudi kwake. Kwetu sisi neno la musingi ni: *"Watoto wa dogo, kaeni ndani yake,"* Niya muhimu sana. Katika Yohana 15:5: Mkombozi wetu alisema, "*…Akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya nen lolote."*

## Leo maandiko haya yametimia

Tunaishi katika siku za wakati wa mwisho mbele yakurudi kwa Yesu Kristo. Tuna ona na macho yetu na kusikiya na masikio yetu namna unabii wa Biblia ukonatimiya kwa wakati wetu – Ikiwa kuhusu kurudi kwa waisraeli katika inchi yao, Ikiwa kuhusu vita na matetesi ya vita, I kiwa kuhusu mitetemeko ya Dunia, Njaa, na magonjwa.Haya yote yalikuwa yalishaka semewa na BWANA wetu katika (Luka 21). Tuna ishi kwa wakati wa joto kali, mabadiliko ya anga, na masumuko ya maumbile ya kila aina. Kwasababu ya virus mupya ambayo ime julikna kwa jina la "Corona" na ime sambaa Duniani pote kilakitu kime badilika na hakita rudi kati hali yake yake halisi tena.

Alama mkuu ya mwisho ya wakati nikurudi kwa watu wa israeli katika inchi yao ya ahadi. *"Maana BWANA atamuhurumiya yakobo atamuchagua israeli tena, naye ata waweka katika inchi yao wenyewe…"* (Isaya 14:1). Maneno haya yametimiya machoni petu. Inchi ya Israeli iliongeza kuweko tangu mwaka ya 1948. Mapatano ya salama ya mashariki yakati ime leta uangalifu mkubwa kama vile yazama. Katika mwaka wa 2020, septemba, umoja wa warabu pamoja na Bahrain Wali weka sahihi mapatano ya usalama pamoja na Israeli, walio jiitiliya "Mapatano ya Abrham," Kama vile Misri walivyo fanya kwa mwaka wa 1979 na Yordani kwa mwaka wa 1994. Inchi nyingi za ki Isilamu pamoja na nyingine zita fuata hapa karibu upesi. Mapatano ya salama Yamwisho itakayo tokeya katika mashariki ya kati, inatarajiwa kupitia upatanisho kati ya Saudi Arabia na Israeli – mpaka hiyo mapatano inayo semwa ndani ya Danieli 9:27 ndiyo ya mwisho.

Baada ya hayo mapatano yote pamoja na Israeli, kupitiya mapatano ya sheria kubwa zilizo kubaliwa duniani pote, hiyo patano iliyo onyeshwa na Danieli, itamalizwa katika mwisho. Wakati ile usalama, ambao itakuwa tu usalama ya uongo, itakuwa imefikika, *"…Wakati wasemapo, kuna amni na salama, ndipo uharibifu uwajiapo kwa gafla, kama vile utungu umjiavyo mwenye mimba wale hakika hawataokolewa…"* (1 Wathesalonike 5:3). Tuna weza kuona mwendeleo ya usalama ikikamata sura yake katika habari za kila siku.

Unyakuo pamoja na mapatano ya usalama utafanyika karibu wakati moja. Pamoja na unyakuo, Wakati ya neema kwamataifa iko nafikiya mwisho, na myaka saba ya mwisho mbele ya kuanza utawala wa miaka elfu. Wakati wa kwanza wa miaka tatu nasu, Manabii wawili watatokea nakuonekana kulingana na Ufunuo 11, kupitiya hao ndipo kuwekwa muhuri kwawale 144 000 kutoka katika kabila 12 ya Israeli kutafanyika. Katikati ya hiyo myaka saba (7) hiyo agano itavunjika, Ziki kuu itaanza, na Yerusalemu itakanyangwa na mataifa yengine mwezi 42 (Ufunuo 11:2).

Kwa kurudi kwa BWANA Ufufuko wa kwanza utafanyika kwawale walio sinziya katika Kristo (1 Wathesalonika 4:13-18). Ufunuo 20:4-6 unaongeya kuhusu ufufuko ya wale walio toka katika

hiyo ziki kuu (ufunuo 7:13-14). Hawa hawana sehemu katika Unyakuo na katika Harusi, Lakini wa takuwa katika utawala wa myaka elfu: *"…Nami nikaona roho zao waliokatwa vichwa kwa ajili ya ushuhuda wa yesu, na kwa ajili ya neno la mungu, na hao wasiyo msujudia yule mnyama, wala sanamu yake, wala hawakuipokea ile chapa katika vipaji vya nyuso zao, wala katika mikono yao; nao wakawa haiwakatawala pamoja na Kristo miaka elfu. <u>Hiyo ndiyo ufufuko wa kwanza.</u> Heri, na mtakatifu niyeye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza, juu ya hao mauti yapili haina nguvu, bali wa takuwa makuhani wa mungu na wakristo, nao watatawala pamoja naye hiyo miaka elfu."* (Ufunuo 20:4-6). Na wengine wote watakuwa na sehemu katika ufufuo wa pili, amboyo tena nihukumu ya mwisho, baada ya myaka elfu. (Ufunuo 20: 11-15)

Hatuitaji kuingilia hizo somo, Lakini tuna weza kuona kwamba mwisho unakaribiya. Tunaitaji waamini wa kweli kuwatayari katika unyakuo (1 Wathesalonika 4:13-18). Pamoja na kila kitu kinachofanyika kwasasa, tuna weza kufanya kama vile BWANA wetu alivyo sema: *"Basi mambo hayo ya anzapo kutokea, changamkeni, mkaviinue vichwa vyenu, kwakuwa ukombozi wenu umekaribia."* (Luka 21:28).

Tunaweza kusema mara zaidi kwamba: Leo maandiko hii namengineyo imetimiya mbele ya macho yetu! Katika Mathayo 24:14 BWANA wetu alisema, *"Tena habari njema ya ufalme ita hubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapo kuja."* Injii ya kweli ya milele ya Yesu Kristo haijawai kuchukuliwa ulimwenguni kama vile ilivyo kwa wakati wetu. Kwa wakati uliyo pita, na hata mbele na zaidi sana tangu uamsho, hapo kume kuwa uamsho za kiroho, Lakini hakuna hata moja ya hizo ambao ilitangaza injili halisi akiwa chini ya upako wa Roho Mtakatifu kama vile mwanzoni, wakati kanisa la agano jipya lilipo anza. Sasa injili inayojaa na mafundiso ya Biblia, kama vile Uungu, Ubatizo wa maji, Meza ya BWANA, inapahswa kuwa kama vile ilivyo kuwa Mwanzoni. Badala ya yote, ina semeka tena ku BWANA wetu na mkombozi: *"Ambaye ilimpasa kupokewa mbinguni hata zije zamani za kufanywa upya vitu vyote, zilizo nenwa na Mungu kwa kinyawa cha Manabi wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu."* (Matendo 3:21)

Kwa wakati wetu, Wainjilisti wengi wame hubiri injili zao wenyewe, Wote waelekea kati mwendeleo waki karsimatic. Ijapokuwa wote walipitiwa na ahadi ya muhimu ambayo ingelipashwa kutimilika mbele ya kurudi kwa Kristo. Kama vile mpango wa Mungu ulivyo anza katika agano jipya na utimilifu wa unabii wa Biblia. Katika Marko 1 tunasoma: *"Mwanzo wa injili ya Yesu Kristo Mwana wa Mungu; kama ilivyo andikwa katika nabii Isaya, Tazama, namtuma mjumbe wangu mbele ya uso wako atakaye itengeneza njia yako* (Malaki 3:1a). *Sikiliza, nisauti ya mtu aliyaye itengenezeni nyikani njia ya BWANA, Nyosheni jangwani njia kuu kwa Mungu wetu* (Isaya 40:3). *Yohane alitokea akibatiza nyikani, nakuhubiri ubatizo wa toba liletao ondoleo la dhambi. Wakamwe inchi yote ya uyahudi, nao wa Yerusalemu wote, wakabatizwa katika mto wa Yordani, wakiziungama dhambi zao*." (Shahiri la 1-5).

Mutu wa Mungu angeliweza kusema kwawale walioamini ujumbe wake: *"Mimi niliwabatiza kwamaji bali yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu."* (Shahiri la 8). Wakati Yesu alipo onekana, alihubiri akisema: „*Wakati umetimiya na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini injili."* (shahiri la 15).

Katika mahubiri yake ya kwanza baada ya umwangaji wa Roho Mtakatifu, Petro alinea maneno yafuatayo akiwa chini ya upako na uonsgozi wa Roho mtakatifu: *"Tubuni mkabatizwe kilammoja kwajina lake Yesu Kristo mpate ondoleo la zambi zenu, nanyi mutapokea kipawa cha roho mtakatifu; kwakuwa ahadi hii nikwa ajili yenu, na kwawatoto wenu, na kwa watu wote waliombali, na kwawote watakaoitwa na BWANA Mungu wetu wamjie*." (Matendo 2:38-39)

Wakati imetimia. Sasa, kwa mwisho ya wakati wa neema, tuko naishi utimilifu wa unabii wa biblia ulio tabiriwa kwa kanisa, kama vile mwanzoni. Kwa mufano, katika Malaki 4:5 inaandikwa: "*Angalieni nitawapelekea Eliya nabii, Kabla haijakuja siku ile ya BWANA, iliyo kuuna kuogafya. Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo watoto iwaelekee baba zao…"*

Kupitiya hudma ya Yohana Mbatizaji, mioyo ya wa baba wa agano la kale iligeukiya mioyo ya watoto wa agano jipya (Luka 1:17).

Kupitiya hudma ya ndugu Branham, Sehemu yapili ilitimiya:Mioyo ya watoto wa Mungu ilirudishwa kuimani ya baba zao mitume huko mwanzoni: BWANA Yesu alishuhudia hii maahadi ya agano la kale katika Mathayo 17:11: *"Naye akajibu akawaambiya, kweli eliya yuaja, naye atatengeneza yote."* Nabi malaki alitangaza akiwa chini ya upako wa Roho Mtakatifu, Mwokozi wetu alishuhudiya akiwa chini ya upako wa Roho Mtakatifu, nawale wote walio fundishwa kweli kweli wakiwa chini ya upako wa Roho Mtakatifu, wanaamini ahadi nakuona utimiliu wake.

Mungu alimuita mtumishi wake nyumbani kwa mwaka wa 1965 Desemba, Lakini tangu wakati ule, Ujumbe halisi wa kibibilia aliyo ileta ime chukuliwa ulimwenguni pote kulingana na Utume wa Mungu. Inaweza semeka tena hapa: Aliye wa Mungu husikia maneno ya Mungu (Yohane 8:47). Ingawaje, Mtu anaweza naye kuuliza*: "Ni nani aliye sadiki habari tuliyo ileta ? Na mkono wa BWANA amefunuliwa nani?"* (Isaya 53:1, Warumi 10:16).

## Hudma Ya Kinabii

Ina maana kubwa kwangu kumjuwa mtu wa Mungu William Branham kwa kipekee kwa Myaka 10, kwa kushuhudia utangazaji wa injili ya Yesu Kristo katika ujao na kazi za kimaajabu za Roho wa Mungu kupitia ku ombeya wagonjwa kwa mikutano yake. Kama kuhusu huduma ya ndugu Branham, niya muhimu kuonyesha Amos 3:7, Kama vile yeye mwenyewe alifanya mara zaidi. *"Hakika BWANA Mungu hata fanya neno lolote, bila kuwafunulia watu wake manabii siri yake."* Hii ukweli wa kiumungu ni ya muhimu sana kabisa.

Mkombozi wetu naye alitangazwa kama vile nabii katika Kumbukumbu La Torati 18:15: "*BWANA Mungu wako atakuondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zako kama niivyo mimi, msikilizeni yeye*." Mtume Petro alishuhudia utimilifu ya ahadi hii katika Matendo 3:22-23 alikuwa ana sema kuhusu Yesu: *"Kwamaana musa kweli alisema ya kwamba, BWANA Mungu wenu atawainulieni nabii, Katika ndugu zenu, kamamimi; msikieni yeye katika mambo yote atakayonena nanyi. Na itakuwa ya kwamba kila mtu asiye*

*musikiliza huyo ata angamizwa na kutengwa na watu wake"*. Isaya 42:1 BWANA, Mkombozi wetu, anaitwa mutumishi: *"Tazama mtumishi wangu ni mtegemezaye; nae atawatolea mataifa hukumu."* Tuna kuta uthibitisho katika Mathayo 12, shahiri la 18: *"Tazama, mtumishi wangu niliye mteua; mpendwa wangu, Moyo wangu uliye pendezwa naye; Nitatiya roho yangu juu yake, naye atawatangazia mataifa hukumu."*

Nabii wa kweli ni mtumishi wa Mungu kupitiya hio hudma ya BWANA ina endeleyaka. Kama vile nabii, anaonaka mambo ambayo Mungu anatarajia kufanya, na tena kama vile mtumishi, anaichukuwaka kwaheshima na kutii. Mimi kwa kipekee nimekwisha kuiona mara nyingi katika hudma ya Ndugu Branham katika mikutano yake Alisema kwake mwenyewe kama vile nabii na vilevile mtumishi. Yale alio yaona katika maono kamavile nabii, alichukuwa utumishi wakati aliombeya wagonjwa, Mara nyingi BWANA alikuwa akimuonyesha huyo mtu, ninani anaye simama mbele yake kwenye mustari wa maombi, mahali walitokea, na magonjwa gani walio nayo. Kama vile mtumishi, alichukuwa utume wake naangeliweza kusema etii kwa Mufano, "Umeponywa kansa." Ndugu Branham alionyesha kwamba ilikuwa hudma moja kama ile ambao BWANA wetu na mkombozi aliyo kuwa nayo kwa wakati wake. Kupitia ufunuo aliweza kuniambia yanayo kuwa kwenye hudma yangu kwa wakati tano tofauti.

Kuhusu karama ya kuona maono, Ndugu Branham alirudilia zaidi akisema kuhusu matukio tatu katika huduma ya BWANA wetu: Wakati alimukuta Petro mara ya kwanza, angeliweza kumuambia, *"Jina lako ni Simon na jina la baba yako ni Yohana."* Angeli weza kumuambia Nathanael, *"Kabla filipo hajakuita ulipokuwapo chini ya mutini nilikuona."* (Yohana 1) Angeliweza kusema namwanamke kwenye mutoni, *"Kwa maana umeskuwa na waume watano, nayule sasa siye mume wako."* (Yohana 4)

Karama moja kama hiyo ilionwa na kusikilikana kwa mwaka ya hudma ya Ndugu Branham. Angeliweza kusema mara nyingi, "ASEMA BWANA…!" Nailikuja kupita mara nyingi, wakati alipo iona. Haiandikwe tuu: *"Yesu Kristo niyeye yule, jana leo nahata milele."* (Waebrania 13:8), lakini alijifunuwa mwenyewe kama vile

mmoja aliye okowa wenye thambi, aliwafunguwa wale waliokuwa wanafungwa, na aliwaponya wagonjwa kwa wakati wetu, Nilishuhudia mimi na macho yangu mimi mwenyewe. Ma milioni ya wa amini yanaweza kushuhudia hili.

Kwa myaka inayopita, tume sema mara nyingi tukirudilia mwito na kutumwa kwa ndugu Branham na mambo ambayo Mungu amefanya katika hudma yake. Siku ya leo ningelipenda kugusia kidogo kwa tukio la februali, 28, 1963, ambalo lilifunuliwa kwa mtu wa Mungu. Ilitendeke kwenye mlima wa sunset huko Arizona, karibu maili 42 kutoka muji wa Tucson: BWANA alishuka katika wingu la kimaajabu, ambalo lilifanyika na malaika Saba (7). Hapo aliambiwa kurudi huko Jeffersonville kwani wakati wa kufunua mihuri saba ilikuwa imetimia. Tangu Machi 17 mpaka 24, 1963, mtu wa Mungu alihubiri kuhusu mihuri saba.

Magazeti mingi ambao niwapasha habari wa USA yaani Marekani, walitoa habari ya wingu kuu la kimaajabu. Ili kuwa ndiyo sije ama habari kubwa ya siku katika wapasha habari, Lakini katika wa pasha injili wote na wa hubiri wote, Ninani aliye shika makini yahiyo mpaka sasa? Wote wana mpango yawo lakini hawajuwe yule ambaye Mungua aliahidi kwawakati hii. Pasipo kuijiwa ako, Wamekataa shahuri za Mungu wakijiheshimu wenyewe, kama vile waongozi wakiroho walifanya huko nyuma. (Luka 7:30). Hivyo ndivyo ilivyo kuwa katika Dunia ya kidini kwakuja kwakwanza kwa Kristo, Nahiyo ndiyo shida nahata sasa, Mbele ya kurudi kwake kwa mara ya pili. Lakini kama vile BWANA alimtume Nabii Yohana huko nyuma kutimiza maandiko nakutayarisha watu wawe tayari kwa BWANA, Ina lingana namtu wa Mungu William Branham alivyo pokea kutumwa kwake, Sauti ya kusikilikana kutoka katika wingu la kimaajabu tarehe 11, Juni, 1933, katika ubatizo ndani ya mto Ohio: **“Kama vile Yohana Mbatizaji alivyo tumwa kutayarisha kuja kwakwanza Kristo, Ndivyo hivyo nawewe umetumwa na ujumbe ambao utatayarisha kurudi kwapili kwa Kristo.”** Siku ya leo tunaweza kusema na ujasiri: kutumwa hii imetendeka.

## Imani ya kweli ni nini ?

Ndugu Branham alihubiri mahubiri tarehe 24, Novemba 1963, inayo itwa: "Aina tatu za waamini". Ndani humo anaongelea kuhusu mwamini wa kweli, na waamini nusu, na wasio amini. Abraham ndiye mfano wa imani ya kweli netena analinganishwa kama "Baba wa waamini wote." *"Maana maandiko ya semaje? Ibrahimu alimwamini Mungu, Ikahesabiwa kwake kuwa haki."* (Warumi 4: 3). Mtume Yakobo alionyesha imani ya kweli pamoja na kuheshimu na kazi na aliandika kwamba imani pasipo matendo nibure. Ali eleza vizuri, *"Je! Baba yetu Ibrahimu hakuhesabiwa kuwa ana haki kwamatendo, hapo alipo mtowa mwanawe Isaka ju ya madhabahu? Waona kama imani ilitenda kazi pamoja na matendo yake, na ya kwamba imani ile ilikamilishwa kwanjiya ya matendo yale. Maandiko yale yakatimizwa yaliyo nena* (Mwanzo 15:6) *Ibrahim alimwamini Mungu, Ikahesabiwa kwake kuwa ni haki; naye aliitwa rafiki wa Mungu."* (Yakobo 2:21-23)

Wakati BWANA wetu anasema, *"Aaminiye nakubatizwa ataoka…"* (Marko 16:16), Hii inaacha wapi hao wanao jilia kuamini nakisha wana kataa ubatizo wa maji? Kwa lengo hili, Imani hainekane katika matendo. Baada ya yote, haiko juu ya kazi zetu ambazo tuna weza kumaliza; Kutii neno inaonyesha imani yetu. Ninamnagani kuhusu wale wanao jitangazia kwamba wanaamini lakini wanakataa yale ambayo BWANA alisema katika utume kubwa kwa mfano ndani ya Marko 16 ? Kwakweli watu kama hao ni wa amini, ama ni wa amini nusu? BWANA wetu alisema, *„Yeye aniaminiye mimi, Kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya…"* (Yohana 14:12) "*…Na hishara hizi zita fuatana na hao waaminio…"* (Marko 16:17). Ni wakati tu BWANA Mungu anaongeya na mtu kipeke kupitiya neno lake na kumpatiya ahadi, hapo ndipo mtu huyu ata amini, atafanya kwa kutii kile ambacho maandiko ina sema, na kuishi katika yale yalio ahidiwa.

Inatuuma sana kusema kwamba hawa waamini nusu wana pita pembeni ya Mungu katika yale wanayo amini na kufundisha katika maombi yao. Watu wanaolinganishwa ku Neno la Mungu lakini wana sikiliza tu mahubiri iliyo undwa na watu katika mikutano yao inayo wa ongoza kuwa waamini nusu. (wanaojiitia),

kama vile ilivyo katika madini yote, niwaamini nusu. Inajulikana vema kwamba makanisa ya kikristo wako na ma kredo zawo wenyewe, nahata wanajiita mitume ijapokuwa hawana hata nakidogo ya fundisho ya mitume. Kwa kuongeza ku wale wanao jiitiliya eti ni "kukili ya kimitume," kuna tena kukili ya Nicene (AD 325) na kukili la Chalcedonian (AD 381), Na mengineo.

Hata hivyo taalimu moja ya imani ya kimitume inakutwa tu ndani ya Biblia kamavile urithi ya agano jipya. Ya fuatayo ikingali na shikilia kweli kwa waamini wa kweli: *"Aniaminiye mimi kama vile maandiko yalivyo nena…"* (Yohana 7:38). BWANA alisema hii kwa wale wote wanao amini mafundisho yao wenyewe: *"Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yalio maagizo ya wanadamu."* (Mathayo 15:9). Hiyo inabaki kweli milele: *"Lakini saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi Wata Mwabudu Baba katika roho na kweli: kwamaana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu."* (Yohana 4:23). Hapa tuna weza ku swali swali kubwa: Kwakweli, tuna mwamini nani? Je, tuna amini yale ambayo Mungu alisema nakuahidi ndani ya neno lake na yale yaliyo fanywa huku kwa ukristo ulio anza, Ao je, tunaamini amri na mafundisho zilizo tengenezwa na wanadamu zinazo fundishwa katika makanisa za kikristo?

Wasio amini haiko tu wale wasioamini kwakweli na wale ambao Mungu hayumo ndani yao. Ya umuhimu mkubwa ni yale ambao mtu wa Mungu William Branham alio iseme kuhusu kutokuamini na anguko la mtu katika paradizo. Hii ni moja ya ufunuo wamuhimu aliyo upokea kutoka kwa BWANA katika uhusiano na mpango wa Wokovu. Kwanza Lucifer alijiinua mbinguni ba alitaka kujilinganisha na yule mkubwa zaidi, lakini alishindwa pamoa na wale wote walio mfata (Isaya 14: 12 – 15). Anguko la mwana damu kaika paradizo lilikuwa wakati tu shetani alimshawishi Eva kupitia mazungumzo shetani akiwa katika umbo la nyoka akiwa na maneno: "Mungu alisema…?" Hiyo kupanda mbegu ya mashaka kwayale ambao Mungu alimuambia Adamu. Hivyo ndivyo kutokuamini iliingizwa, ambayo ilizaa kuto kutii, Nakupitiya hiyo upotevu, mwanadamu yeyote alikokotwa katika anguko na hapo kifo kika ingizwa. Kutiya mkazo katika imani ya kweli, mwokozi wetu alisema, "…*kwasababu*

*msipo sadiki ya kwamba mimi ndiye, mtakufa katika dhambi zenu.”* (Yohana 8:24). Nahata sasa imani ya kweli inapashwa kuwa nanga ndani ya wale wanao amini ndani ya Yesu Kristo na yale ambayo Mungu ali nena katika neno lake. kutokuamini kila wakati ina letwaka na mbegu ya Mashaka ambayo muovu anapandaka.

Acheni kila mmoja ajichunguze mwenyewe, kuona kama kwakweli yeye ni muamini wakweli kulingana namaandiko na anaamini kila neno la Mungu na moyo wake wote, Na anakubali kila ahadi yote ambayo BWANA alifanya, na anafungwa kilindini pamoja na Mungu. Waamini wa kweli nisehemu ya wachaguliwa, wamezaliwa marayapili naneno pamoja na Roho wa Mungu, na wanaongozwa ndani ya kweli yote. Wanaamini katika mwito wa kiungu wa Ndugu William Branham, aliye leta ujumbe wakibiblia, aliyetangaza vivyo hivyo ulimwenguni pote.

Waamini wa kweli wamekwisha tambua wakati na saa ambayo tunaishi wame kwisha kutoka ndani ya mafundisho ya kidini, Katika mafundisho zote zisizo za kibilblia na wametakaswa na neno la kweli. Ombi la mkombozi wetu ni: *“Uwatakase kwakweli neno lako ndilokweli”* (Yohana 17: 17). Hiyo inaanza pamoja na Uungu: Mafundisho ya kweli inashuhudia Mungu mmoja. Hakuna hata maramoja neno la “ Utatu” ao “ Mungu kwa wa tatu” inayo patikana katika Biblia. Hata hakuja hwai kuwa swali la watu watatu wa milele. Biblia inajua tu Mungu mmoja aliye tangaza mpango wa ukombozi na akayifanya (Akayitimiza) yeye mwenyewe. Alijifunua kama Baba ndani ya mbingu, katika mwana wake alie mzaa Yesu – Kristo (“EMMANUELI” = Mungu pamoja nasi) duniani na anatumika na Roho mtakatifu ndani ya kanisa ya walio kombolew. Hakuna hata maramoja matamko ya “ Kwa Jina la Baba, Kwa Jina la Mwana, Kwa Jina la Roho Mtakatifu” Haija tumikishwa katika Biblia.

Vilevile kuhusu Ubatizo, kunafanyika yale ambayo Petro aliagiza siku kanisa la Agano Jipya lilipo anza (lilipo anzishwa) akiwa chini ya upako wa uvuviyo wa roho mtakatifu (Matendo 2:38-41) Petro alitimiza utaratibu wa utume na alitumika kwa ujasiri, kama vile Filipo vilevile (Matendo 8:16) na Paulo (Matendo 19:5) vile na waamini wote katika kizazi cha kwanza, wakibatiza

waamini wakwanza walio kubali ndani ya Jina la BWANA Yesu – Kristo. Kwakuwa ni Jina, ambalo Mungu amejifunuwa ndani yake kwetu katika Mwana, kama Baba na Roho mtakatifu. Neno la Waefeso 4:5 ni wazi hata Leo: *"Bwana mmoja, Imani moja, Ubatizo moja…"*

Wale wote wanao amini kikweli, ni watiifu na wanaishi kwa yale yanayo andikwa katika 2 Wakorinto 6:17-18: *"Kwa hiyo tokeni kati yao, mkatengwe nao, asema BWANA, msiguse kitu kilicho kichafu, naminitawa karibisha. Nitakuwa Baba kwenu nanyi mutakuwa kwangu wana wa kiume na wa kike asema BWANA mwenyezi."* Niwale watakao fikia mwisho ya kazi kupitia kitendo chakimbinguni cha roho matakatifu. Bwana mungu atatuma mvua ya kwanza na ya mwisho kwanguvu nyingi, kama ilivyo tabiriwa na mtume Yakobo chini ya upakoo wa uvuviyo wa roho mtakatifu: *"Kwa hiyo ndugu, vumilieni, hata kuja kwake BWANA. Tazama mkulima hungoja mazao ya nchi yalio ya thamani, huvumilia kwa ajiliyake hata yatakapo pata mvua ya kwanza na ya mwisho."* (Yakobo 5: 7). Lakini nabii Yoweli alikuwa chini ya upako na uvuviyo wa roho mtakatifu: " *Furahini, basi, enyi wana wa sayuni, mkamfurahia BWANA, Mungu wenu, kwakuwa yeye huwapa ninyi mvua ya masika, na mvua ya vuli, kama kwanza…"* (Yoeli 2:23)

Nakama vile mtume Petro aliiandika tunaweza kufurahia hili: *"Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani hata mpaye wokovu ulio tayari kufunuliwa wakati wa mwisho."* (1 Petro 1:5) Tumezifikia siku za mwisho kwahivi tuna pashwa wa angalifu na watu wazima kwakila jambo nakunyenyekea kwa kila hali tunayo weza kutana nayo, ilikusema tusiweze kuhayarisha jina la BWANA wetu Yesu.

Ninge penda nionyeshe maramoja tena kwamba hakuna mtu hatu mmoja alie ndani ya uongo Kupitia mafundisho mabaya atakaye ingia Mbinguni. BWANA alifanya neema kwakuturudisha kwa mungu, kwaneno lake, na kwafundisho lamitume kupitia ujumbe wa mwisho, unayo fanana na ule wa kwanza kabisa. Yeye asiye hiyo, hakutambua siku ya kutembelewa ya Mungu (Luka 19: 42-44).

Katika Luka 21, BWANA alitangaza mambo mengi yanayo timia na akasema kulingana nasiku za mwisho: *"… na mataifa wakishangaa kwa uvumi wa bahari na masukosuko wake; watu wakivunjika mioyo kwa hofu … Basi mambo hayo yaanzapo kutokea, changamkeni, mukaviinue vichwa vyenu, kwa kuwa ukombozi wenu umekaribia … Nanyi muonapo mambo hayo yanaanza kutokea tambueni ya kwamba ufalme wa Mungu u karibu … Basi, kesheni ninyi kila wakati, mkiomba, ilimpate kuokoka katika haya yote yatakayo tokea, na kusimama mbele za Mwana wa Adamu."* (Luka 21:25-36). Ametupatia ahadi: *"Na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."* (Matayo 28:20)

Ndugu Branham alitumika utume wake wa kinabii na aliweka kwa Ghala chakula cha kiroho. Na mimi pia nilifanya yale ambayo BWANA ameni agiza, Kwakuweka neno la unabii kulingana na mafundisho, na kwakugawa chakula cha kiroho kama vile BWANA alishuhudia tarehe 19 septemba 1976 (Matayo 24:45-47). Kwa neema ya Mungu, Niliweza kuweka vizuri ndani ya neno la Mungu ma nukuu zote zilizo ngumu kwakuelewa za ndugu Branham. Hivyo ndivyo Petro aliandika kwa wakati wake akilinganisha na mabaruwa za Paulo*: "Katika katika nyaraka hizo yamo mambo ambayo nivigumu kuelewa nayo, na mambo hayo watu wasiyo na elimu, wasio imara, huyapotoa, kamavile huyapotoavyo na maandiko mengine, kwa uvunifu wao wenyewe."* (2 Petro 3:15-16). Nina weza kushuhudia, kwakuwa nime yafanya yale ambayo Paulo aliyo yaandikia Timoteo wakati wingine: *"Lihubiri neno, uwe tayari,wakati ukufaao na wakati usiyo kufaa, kalipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho"* (2 Timoteo 4:2), kama vile BWANA alivyo niagiza kwasauti kubwa huko Marseille. Hiyo ndiyo sababu, ninahubiri neno pekeyake nakuyatupilia mbali matafsiri yoyote.

Vile kama Paulo, naweza sema pia: *"Lakini BWANA alishimama pamoja nami akanitia nguvu ili kawa kazi yangu ule ujumbe utangazwe kwa utimilifu, hata wasikie mataifa yote."* (2 Timoteo 4:11)

Wandugu wotw wenye huduma kwakweli kutoka kwa Mungu wana gawa chakula cha kiroho: Neno safi lenye kufunuliwa. Meza

ya BWANA, haija wai kujaa chakula, kama vile ilivyo kwa wakati wetu. Sasa tuna pashwa, Kuungana katika maombi kwakutetemeka na BWANA mwenyewe atamaliza kazi yake ya ukombozi na nguvu kubwa (Waroma 9:28). Na kwa mwisho, itakuwa kama vile Ndugu Branham alivyo ona, Bibi Arusi atarembea kwa hatuwa moja kwa Kiroho na Mungu atajibu maombi yetu, kwa ginsi yale ambayo tutasema kwa imani yatatimia. Iliyo ya muhimu ni kwani tutadumu ndani ya Neno na ndani ya Mapenzi ya Mungu, kwakuwa ni kwanamna hii ambayo anaweza kupendezwa na sisi.


## Myaka 70 imepita

Siku ya Pentekoste ya mwaka wa 1949, nilitakasia maisha yangu kwa BWANA Yesu na machozi ya kutubu nanilipokea ubatizo Roho mtakatifu. Tangu wakatiule minaweza kuona nyuma nakuona njia ya imani inayo barikiwa na BWANA kwa ujao. Kwa neema ya Mungu nilihubiri Neno la Mungu tangu 1952 kwa Kanisa la Kipentecoste.

Nilishirii kwa mukutano ya ndugu Branham aliyo ifanya huko Karlsruhe, huko Ugerumani kwa mwaka wa 1955. Kwa mkutano yake ya kwanza, nilitambuwa ya kwamba alikuwa mutu wa Mungu na kwamba alikuwa na huduma isiyo ya kawaida ambayo inafungwa kwa mupango ya okovu wa Mungu kwa wakati wetu.



Rev. Branham spricht im



Bis zu 10000 Zuhörer füllten und umsäumten in einer Versammlung das Karlsruher Branhamzelt

**Picha hapo chini inaonyesha moja ya mkutano abazo zilifanyika huko Hallenstadion katika Zurich Switzerland, kutoka Juni 20-26, 1955; ile yengine picha inaonyesha mkutano wa Karlsruhe, Ujerumani, hapo Ndugu Branham alihubiri kutoka Ogosti 12 mpaka 19, 1955.**

Kupitia chini ya uongozi wa Mungu, tulianza kwa mwaka wa 1958 kutafsiri mahubiri ya ndugu Branham, zilizo kuwa kwenye kanda nahapo ndipo kanisa la pahali lili anza kuonekana linalo jitawala nakwakufuata kazi ya umishonari. Tarehe 2 Aprili 1962, nilipokea mwito wangu kupitia sauti ya BWANA inayo sikilikana. Hili lilishudiwa na ufunuo wa kiungu wa tarehe 3 Disemba 1962 na



Hallen-Stadion in Zürich

ndugu Branham alie nipatia maagizo mengine kwa upande wa BWANA ambayo yanafungwa kwa utume.

Kwa mwaka wa 1964, Nilianza safari yangu ya kwanza ya umishonari huko india nanilitembelea Yerusalemu kwanjia ya kurudi. Kuanza kwa mwaka wa 1966 nilianza na safari za kimishonari ndani ya mainchi jirani na pia Duniani. Kwa ajili ya





**Picha hizi mbili kutoka mwaka wa 1976, moja kutoka Zurich, Switzerland, na engine kutoka Heilbronn, Ujerumani, inaonyesha namna Mungu alibariki utangazaji wa Neno Lake.**

mahubiri niliyo kuwa nikihubiri muda wa dakika 20, kwa njia ya Radio huko Luxembourg kwa mwaka wa 1967 na 1978, Niliweza kufikia wasikilizaji wengi wa lugha za kijerumani na kwa namna hiyo niliweza Kuwaalika kwenye mikutano ya miji mbali mbali. Hesabu ya waamini wengi waliokuwa kwenye mikutano hiyo yenye baraka waliyo yihuzuriya pamoja na ndugu Branham, kwa kitendo hicho, chumba yote ilikuwa ikijaa kwakila muji, ikiwa Uswisi, huko Autriche ao ujerumani. Ilikuiwa myaka yenye baraka sana, katika ufalme wa Mungu.

Kwa mwaka wa 1979, Adui alipata namna ya kuusambaza mashaka, kama vile ilivyo kuwa kwa Hawa kwenye paradizo, pamoja na swali: “BWANA kwa kweli aliongea naye?“ Hivyo ndivyo jinsi utume uliwekwa kwa maswali na hiyo iliongoza mpaka kufikia kubomolewa kwa kanisa la mahali. Lakini BWANA Mungu alionyesha ushindi wa Golgota; Wateule hawakuanguka ndani ya kudanganwa na huduma iliendelea mpaka leo.

Kwa mwaka huu wa 2020, Nimeongozwa kutopanga safari hata moja ya kimishonari. Na ginsi tulichunguza, tuliona kwamba haingewezekana sababu ya magonjwa ya VIRUSI Vya COVID 19. Na kwasababu hiyo, hatukuweza kufanya mikutano ya watu kutoka inchi mbalimbali, hapa kwenye kituo cha misheni cha Krefeld wakati huu. Tuna shukuru Mungu sana kuona tangu 1974, Ma millioni ya waamini wa dunia mzima waliweza kusikia neno la Mungu hapa, kwachumba chetu cha kukusanyika. Kile BWANA aliniangiza kimetimia: “Ni kusanyisheye watu pamoja, kusundi walisikilize maneno yangu.”

Vilevile ginsi ameshugulikia uwekaji na ugawaji wa chakula cha kiroho, Ni hivyo hivyo pia ndivyo alivyo shugulikia ili mwito wa ujumbe wa mwisho wakutoka na wakurudishwa uwezekusikilikana kwa njia ya INTERNETE. Mungu akipenda nitakuwa nina hubiri kila juma pili ya Mwisho ya mwezi, hapa krefeld na saa inne (10:00) ile inayo julikana kama juma pili ya Zurich iliokuwa inafanyika kila juma pili ya mwisho ya mwezi pa saa nane (14:00) na kila juma pili ya kwanza ya mwezi na 10:00. Mahubiri haya yanatafsiriwa kwalugha mbali mbali, na zina tumwa kwa njia ya INTERNET,

mahali ambapo yanasikilizwa kila mahali duniani kwa maeneozote, na mielekeyo (ao njia) zinazojulikana.

Kwa namna nyingine tuna tuma mahubiri kila siku yatatu nasiku ya sita mangaribi, na siku ya juma pili asubuhi, (Kulingana na Orotha ya ulaya ya kati) mahubiri ya myaka 1980. Mahubiri hayo yana tafsiriwa pia kwalugha mbali mbali kwa ginsi wa Amini, hata vilevile makanisa yote kwajumla, yanaweza kufungwa hapo kenye mtandao katika dunia nzima.

Mahali ambapo inawezekana wandugu ndani ya hudma wana weza kuendelesha mikutano za pahali. Mahali pote duniani, wakati waamini wanapo kusanyika kwa jina la Yesu Kristo, BWANA yuko kati yao (Matayo 18:20). Nina wasihi mkamate maneno haya kwa mioyo na ku ya amini. Wakati unakuja ambao kila waamini wa kweli, ao ikiwa duniani, wanakusanyika katika maombi, ili BWANA Mungu aweze kutumikia mahali pote, kumaliza kazi ndani yawale walio kombolewa na matayarisho ya kanisa bibi arusi.

Wale wote wanao amini sasa neno lililo funuliwa hao ndiyo wenye kufanya sehemu ya Mabikira wenye busara na wanaishi katika matayarisho ya mwisho kama kanisa bibi arusi, kwakuwa inaandikwa: *"… nao wale waliokuwa tayari wakaingiya pamoja naye arusini, mlango ukafungwa…"* (Matayo 25:10). Kwa hii kunafungwa ufunuo 19:7: *"…na bibi arusi wake ame jiweka tayari…"* Yeye ana ukobozi mkamilifu kupitia damu ya mwana kondoo (Matayo 26:28), anautakaso kamilifu kupitia neno la mungu (Yohana 17:17) na atawekwa muhuri na amewekwa muhuri wa Roho Mtakatifu kwa siku ya ukombozi wa mwili yake, Kulingana na neno la waefeso 1:13: *"Nanyi pia katika hiyo mumekwisha kulisikia neno lakweli, habari njema za wokovu wenu; Tena mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa muhuri na roho yule wa ahadi aliye mtakatifu."*

Nina weza kuona nyuma kwamyaka hiyi yote iliyo pita, naninashukuru kwa mara nyingi niliyo itwa na BWANA na kunipatia maagizo. Alifanya mambo makuu mbele ya mamilioni ya watu akiwarudisha kwenye imani ya kweli. Kama wakati mwingine Simeoni (Luka 2:29), nina weza kusema nazamiri nzuri: "Sasa, BWANA, mruhusu mtumishi wako kwa amani, kwakuwa maacho

yangu yameona jinsi mataifa yote ya Dunia nzima ya mesikia ujumbe wa kimisingi ambao unatangulia kuja kwa pili kwa Kristo."

Kwa mwaka ujao tunangojea yubile ya kweli, ambayo imetangazwa na BWANA katika Luka 4, na hapo ndipo kila mmoja ataingiya kwa urithi wa yale ambayo Mungu ametupatia: *"… na ku watangazia uhuru watu wote katika nchi; itakuwa ni mwaka wa yubile kwenu; nanyi kila mtu atairudia milki yake mwenyewe nanyi mtarejea kila mtu kwa jamaa yake."* (Walawi 25: 10).


*"Nasi tunajuwa yakuwa katika mambo yote mungu hufanya kazi pamoja nawale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake. Maana wale alio wajuwa tangu asili, aliwachaguwa tangu asili wa fananishwe na mfano wa mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwandugu wengi. Nawale alio wachagua tangu asili, hao hao akawaita; nawale alio waita hao akawahesabia haki; nawale alio wa hesabia hake ; hao akawatukuza."* (Waroma 8:28-30).

Muni fikilie mimi na wandugu wote ndani ya hudma katika maombi yenu.

Inafanyika kwa upande wa Mungu

Bro. Frank

# THE 70 WEEKS OF DANIEL







The faithful LORD sent the prophet to bring the message. HE also ensured that it was carried into the entire world. HIS promise has been fulfilled before our eyes: *"And I saw another angel fly in the midst of heaven, having the everlasting gospel to preach unto them that dwell on the earth, and to every nation, and kindred, and tongue, and people …"* (Rev 14:6).

It has reached the ends of the earth, and the LORD will complete His work of redemption (Mat 24:14). To Him alone be the glory through Jesus Christ, our LORD.